

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Telegrams "REGCOM" Shinyanga
Simu Na: 028 - 2762222
Fax Na: - 2762310
Barua pepe: ras.shinyanga@tamisemi.go.tz
ras@shinyanga.go.tz
Tovuti: www.shinyanga.go.tz



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
S. L. P 320,
Shinyanga

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**YAH: ZIARA YA SIKU MOJA YA MHESHIMIWA
KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (MB), WAZIRI MKUU
WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA
MKOA WA SHINYANGA**

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa anatarajiwa kufanya ziara ya siku moja katika Mkoa wetu tarehe 09 Agosti, 2019.

Akiwa Mkoani hapa, Mheshimiwa Waziri Mkuu atakagua na kufungua Ofisi 8 za Tarafa zilizojengwa kwa fedha ya Serikali Kuu, kwa kutumia mfumo wa "Force Account" na usimamizi mzuri wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Ofisi hizi zimekamilika kwa muda mfupi kwa asilimia 100.

Aidha, Mheshimiwa Waziri Mkuu atatembelea na kuona nyumba 10 za makazi ya Askari Polisi, zilizopo eneo la Kamarage na kutembelea kiwanda cha kuchambua Pamba cha FRESHO eneo la Ibadakuli.

Katika maeneo hayo yote, Mheshimiwa Waziri Mkuu atapata nafasi ya kusalimiana na Wananchi wa Mkoa wa Shinyanga.

Baada ya shughuli hizo, Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa amehitimisha ziara yake katika Mkoa wetu.

Hivyo, ninawaomba wananchi wote mjitokeze kwa wingi kumlaki na kusalimiana na Kiongozi wetu katika maeneo yote atakapopita.



Zainab R. Telack
Mkuu wa Mkoa
Shinyanga
07/08/2019